



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Simu: 0232935443
Nukushi: 0232935442
Baruapepe:td@[nanyambatc.go.tz](mailto:td@nanyambatc.go.tz)

2 Barabara ya Bomani,
S.L.P 1490,
63682 NANYAMBA-MTWARA

02/05/2024

TAARIFA KWA UMMA.

BARAZA LA MADIWANI LAMFUTA KAZI MTUMISHI NANYAMBA.

Menejimenti ya Halmashauri ya Mji Nanyamba inapenda kuutarifu Umma kuwa Baraza la Madiwani katika mkutano wake wa tarehe 30/04/2024 lilifanya maamuzi ya kumfukuza kazi katika Utumishi wa Umma **Ndg. Issa Ayub Bangula**, aliyekuwa **Daktari Daraja la II** katika Kituo cha Afya Dinyecha kwa mujibu wa kifungu cha 6(1) (b) cha sheria ya Utumishi wa Umma namba 8 ya mwaka 2002 iliyorejewa mwaka 2019 kwa kosa la utoro kazini.

Kufuatia uamuzi huo uongozi wa Halmashauri ya Mji Nanyamba unapenda kuisisitiza kwamba Halmashauri haitahusika kwa namna yoyote na shughuli au makubaliano yoyote yatakayofanywa na aliyekuwa mtumishi tajwa hapo juu kwani Utumishi wake umekoma tangu 30/04/2024.

Imetolewa Na;



Monica P. Makuluni,
**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO YA SERIKALI,
HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA**